*Mulika, Na. 41 (2), 242-262*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Nafasi ya Nyimbo katika Ufundishaji wa Msamiati wa Kiswahili kwa Watoto wa Elimu ya Awali

*Tumaini Samweli Mugaya*[1]
Chuo Kikuu cha Dodoma

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na41t2.8

**Ikisiri**

Lengo kuu la makala haya ni kuonesha nafasi ya nyimbo katika ufundishaji wa msamiati wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa watoto wa elimu ya awali. Utafiti huu umeonesha kupandikiza hali mpya ya matumizi chanya ya nyimbo kwa walimu na watoto katika utoaji na upokeaji wa elimu. Mkabala wa kitaamuli umetumika kubainisha data katika mada ndogondogo. Usampulishaji lengwa ulitumika kuwapata watoataarifa 20. Nadharia ya Vygotsky ya Ujenzi wa Jamii imetumika kuonesha kuwa nyimbo na msamiati wa lugha ni tendo la kijamii katika kutolea maarifa. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba kuna uhusiano mkubwa baina ya nyimbo na ufundishaji wa msamiati wa lugha. Imebainika kuwa nyimbo ni njia muhimu ya mawasiliano miongoni mwa wanajamii. Njia hii hutumika katika miktadha mbalimbali ikiwa na dhima ya kuburudisha au kufikisha ujumbe fulani katika jamii. Hii ni njia nyepesi na rahisi zaidi kwa watu hususani watoto kwani nyimbo huwashirikisha pamoja kupata uelewa wa msamiati na kile mtoto anachofundishwa kupitia uimbaji. Hivyo basi, nyimbo zina nafasi kubwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa msamiati katika kuijenga lugha ya Kiswahili na kuendeleza maarifa ya watoto. Aidha, nyimbo huleta motisha na huwajenga watoto kiakili, kihisia, kimwili na kijamii katika kutafsiri maisha yao ya baadaye.

## 1.0 Utangulizi

Kuna uhusiano mkubwa kati ya nyimbo na suala la ujifunzaji msamiati wa lugha. Kutokana na umuhimu huo, makala haya yanalenga kuchunguza dhima ya nyimbo katika kuhamasisha watoto katika ujifunzaji wa msamiati wa lugha ya Kiswahili. Aidha, katika sehemu hii ya utangulizi mwandishi amejadili uhusiano wa nyimbo na lugha, na pia ameonesha jinsi masuala ya lugha, nyimbo/fasihi simulizi yanavyotiliwa mkazo katika mitalaa ya elimu nchini Tanzania. Kwa kufanya hivyo, imebainika waziwazi kuwa nyimbo zina nafasi kubwa sana katika kumlea mtoto na kumpatia stadi muhimu za kuifahamu lugha yake.

[1] **Baruapepe:** *samwelimugaya84@gmail.com*

## 2.0 Lugha na Nyimbo

Tafiti zinaonesha kuwa nyimbo na lugha ni mambo yenye uhusiano wenye mshikamano mkubwa. Kutokana na uhusiano huo ni vigumu kujadili kimojawapo bila kuhusisha na kingine. Hii ni kwa sababu wimbo unafikisha ujumbe kwa kutumia lugha (Davanellos, 1999; Arevalo, 2010). Kwa mfano, Davanellos (1999) anaeleza kuwa nyimbo zinapotumiwa katika hatua za awali za ufundishaji, husaidia kukidhi hitaji la kutoa maelezo ya awali ya wazo kuu, kujenga misingi ya kiisimu, kuelimisha na kumwandaa anayejifunza kisaikolojia katika utendaji. Nyimbo zina dhima za msingi katika kila hatua ya maisha ya binadamu (Esimone, 2012). Nyimbo huakisi utamaduni, historia, visasili, visakale na lugha katika jamii au taifa.

Uimbaji ni nyenzo mojawapo muhimu katika kuwajenga wanafunzi wajielewe na wajiamini. Njia hii inapotumiwa na watoto huwafanya waweze kutoa sauti igizo kwa mfululizo wa namna wanavyozisikia kabla hawajaanza kuzitamka. Wanaposikia maneno yanayotamkwa kwa matumizi anuwai, watoto huyatamka vilevile wakiyajenga katika muktadha wa tungo pia katika uimbaji wa nyimbo wanazozisikia. Wanaposikiliza nyimbo mbalimbali, watoto hujifunza msamiati unaowajengea dhana kadhaa na hivyo kuimarisha uwezo na umilisi wao katika lugha.

Tafiti tangulizi zilizofanywa kuhusiana na nyimbo zimesisitiza kwamba nyimbo ni kazi za sanaa zenye mfumo wa mahadhi ya sauti zenye mpangilio maalumu wa kupanda na kushuka zikibeba lugha na kuitambulisha jamii (Mulokozi, 1996; Wamitila, 2003). Wanazuoni hawa katika moja ya hoja zao wameonesha kwamba nyimbo ni kipengele cha fasihi simulizi kinachotumiwa katika thamthilia kwa malengo ya utambaji. Mtambaji anatumia nyimbo kuibua dhamira mbalimbali ikiwamo ile ya umuhimu wa elimu.

Kwa mfano, Wamitila (2003) anaeleza kuwa nyimbo huwa na mawazo mazito na hukusudiwa kuonesha uhusiano wa kijamii, mgogoro, kukejeli, kuliwaza, kubembeleza, kutumbuiza, na kuburudisha. Mawazo haya yanatuelekeza katika kuziona nyimbo katika uwanja wa fasihi tu, na kazi kubwa ikiwa ni kuburudisha. Jambo hili ndilo lililomsukuma mwandishi kuandika makala haya ili kupanua wigo wa matumizi ya nyimbo katika vipengele vingine vya sarufi ya lugha na uamilifu wake katika ufundishaji darasani.

Makala haya yamebainisha kuwa nyimbo hazitoi mawazo mazito na kuburudisha tu, bali ni chanzo cha mazoezi ya lugha kwa mtoto na zinaweza kutumiwa kufundishia msamiati kwa namna zinavyotumiwa na mwalimu vizuri darasani akijenga motisha katika kutolea maarifa. Kazi hii imejadili kwamba kadiri mtoto anavyozitumia nyimbo hizo, ndivyo anavyoielewa lugha kupitia sauti za nyimbo anazozisikia ili abainishe msamiati na kuimudu lugha tangu anapozaliwa akilelewa na wazazi wake hadi anapokutana na walimu shuleni.

Nyimbo hubeba mada za mafunzo na kuijenga sarufi ya lugha (Schmitt, 2010), kumbukumbu (Vygotsky, 1980) na hali, furaha na motisha (Martin, 2013). Nyimbo zinapotungwa vizuri kwa sauti tamu na maneno ya mwendo mzuri wa mapigo, huwajengea watoto uwezo mkubwa wa akili katika kukumbuka. Hivyo, tukihusisha muziki na lugha tunapata mchachato unaowezesha kujifunza msamiati na tungo. Tunapotumia nyimbo kufundisha msamiati, tunaanza kwa kuzisikiliza na kumalizia mawasiliano. Kwa mfano, mtoto asiyejua lugha ya Kiswahili atapata matatizo ya kujieleza, lakini anapotumia nyimbo anaweza kujifunza vizuri lugha endapo atazitumia vizuri kwa namna itakayompa mazingira huru ya uelewa. Hivyo basi, nyimbo ni zana nzuri katika kufundishia lugha.

Maneno ya nyimbo hutoa msamiati uliokusudiwa, sarufi na namna nzuri za wanafunzi kujifunza. Kwa kusikiliza nyimbo za Kiswahili, wanafunzi wanaweza kusikiliza utamkaji asilia na kuendeleza stadi ya usikivu. Melodia za nyimbo na ridhimu huendeleza stadi nzuri za utamkaji na kumfanya mwanafuzi atamke kama mwenyeji asilia (Kasuwan na Chatuphot, 2013). Namna hii ya kujifunza kupitia nyimbo ni njia yenye ufanisi ya kufundishia msamiati kama vile utumizi wa maneno ya nyimbo unaozingatia utamkaji, mkazo na toni. Uimbaji wa nyimbo kwa watoto wakati wa kijifunza katika mazingira rafiki, huwajengea athari chanya katika maendeleo yao ya lugha (Prescott, 2005; Schmitt, 2010).

Kwa mujibu wa Prescott (2005), muziki ni uga muhimu katika elimu. Haumsaidii mwanafuzi katika kupata maarifa pekee, bali humsaidia pia kuongeza ufaulu wa alama. Kuna tafiti mbalimbali zinazoonesha muziki kuwa na matumizi yenye matokeo chanya darasani. Kama mwanafunzi hafahamu maana ya msamiati fulani, anaweza kupata maana yake katika mistari ya tungo za maneno ya wimbo. Hata hivyo, endapo kuna nyimbo pendwa zilizorekodiwa katika kanda za video, nyimbo hizo husaidia wanafunzi kuelewa maana ya maneno.

Muziki katika kanda za video hutoa simulizi ambazo husaidia kujifunza maneno katika miktadha mbalimbali. Watoto wanaposikiliza nyimbo kwa kuzirudia mara kadhaa, hali hii huwapa taswira katika kujenga maana kupitia maudhui ya kanda za video (Kasuwan na Chatuphot, 2013). Naye Thornbury (2002) anasema kuwa namna hizi zote humfanya mwanafunzi kujifunza msamiati mpya kwa namna asilia ya kawaida wakati wakiimba na kusikiliza nyimbo.

Hii inamaanisha kuwa pale watoto wanaposikiliza na kuimba nyimbo wanazozipenda, huwafanya wapendezewe na kupata motisha katika kujifunza msamiati. Kanda za muziki wa video zilizoandaliwa kufundishia ni ala inayowajengea wanafunzi motisha, kujifunza nyimbo mpya na kupata msamiati pia kuwafanya watoto waelewe kinachoendelea maishani mwao (Tassoni na Karen, 2000; Martin, 2013).

## 3.0 Mitalaa ya Elimu Nchini Tanzania na Suala la Lugha

Miaka ya awali ya maendeleo ya ukuaji wa binadamu ni muhimu katika kujifunza kwake (Esimone, 2012). Mtoto anapolelewa tangu utotoni huimbiwa nyimbo kwa namna ambayo huanza kujifunza msamiati wa lugha kupitia yale anayoyasikia (Murphey, 1992; Ekpo, 2008; Esimone, 2012). Maelezo yanayotolewa na wataalamu hawa yanadhihirisha kwamba nyimbo zina nafasi kubwa katika malezi ya watoto. Malezi hayo hufanywa kupitia nyimbo bembelezi ambazo humkuza mtoto kifikra, anapoitumia lugha kwa ufanisi na kujenga vionjo vyenye hisia vinavyomjenga ili kupata stadi za kijamii. Yote hayo ni muhimu katika malezi na makuzi ya mtoto. Blacking (1973) anadai kwamba muziki ni sauti zilizopangiliwa zinazoweza kuibeba lugha. Naye Walker (1998) anaongezea kuwa sauti za muziki huwa na majibizano hai ya lugha za binadamu yanayoleta mchangamano ili kuelewa, kuhisi, kutambua na kubainisha ujumbe unaolenga kubadili tabia katika kujifunza mambo maishani na kuyaelewa.

Esimone (2012) anasema kuwa muziki unapokuwa katika mfumo wa wimbo haulengi kufurahisha tu watu wengi bali huwafanya wawasiliane na kuwawezesha kutoa fikra huru. Pia, nyimbo huwaunganisha watu na zaidi ya yote huwapa namna nyepesi ya kufundisha na kufunza maarifa kwa watoto wao. Agu (2006) anadai kwamba nyimbo ni muziki wenye ujumi wa kisanaa unaounganisha sauti nzuri zenye mpangilio unaosikika vizuri sikioni na unaoshawishi mwili wakati wowote na mahali popote. Nguvu ya melodia na maneno ya nyimbo hushawishi watu kufanya maamuzi yanayotegemea mahitaji yao.

Nyimbo katika malezi ya watoto na mwendelezo wake katika tendo la kuzifunza darasani ni zawadi ya kisaikolojia kwa watoto ambayo huipenda na kuwajengea haiba. Nyimbo zina nguvu ya kushawishi, hujenga hisia na matamanio kwa watoto. Unapomwimbia mtoto mwenye njaa, unamfanya anyamaze na kuanza kusikiliza sauti tamu zenye maneno ya muwala zinazomfanya aanze kutabasamu na kugugumiza sauti anazozisikia. Ukiendelea kumwimbia zaidi, mtoto anaweza kupata usingizi, jambo ambalo linaufanya muziki uonekane kuwa na nguvu zaidi. Hivyo, kadiri mtoto anavyoupenda wimbo na kuuimba ndivyo anavyoimarisha msamiati na kuimudu lugha.

Utoto ni kipindi muhimu katika maendeleo ya binadamu. Umri wa kuanzia kutungwa mimba, kuzaliwa hadi miaka minane ni muhimu katika ukamilifu wa maendeleo ya mtoto kiafya, kiakili, kihisia, kimwili (Suyanto, 2007). Kipindi hiki cha maendeleo ni muhimu pia katika kuwajengea watoto msingi wa maisha yao na elimu. Tafiti zinaonesha kuwa nusu ya maisha ya akili ya mtu huwa imeendelezwa hadi kufikia miaka minne na kwamba kuwapo kwa uendelezaji fanisi tangu utotoni huathiri uwezo mzuri wa kifikra, haiba na tabia amilifu za kijamii maishani (Thornbury, 2002). Hivyo, taratibu zote za mafunzo katika umri huu ni muhimu katika kuwajenga watoto kiakili na kuitumia lugha katika kijamii yao.

Mwaka 1967 Tanzania ilijielekeza katika mfumo wa elimu ya kujitegemea katika ngazi zote za elimu (Nyerere, 1968). Katika elimu ya awali na shule za msingi, mtalaa ulielekeza ufundishaji ambao uliweka mkazo katika mwegamo kwa mtoto na siyo mwegamo kwa mwalimu wakati wa ufundishaji katika mawasiliano darasani. Hali hii ililenga kuwafanya watoto wajifunze kwa kujitegemea, watende wenyewe binafsi na kujiamini wakati wa kujifunza (MOEC, 2005) na kupendekeza matumizi ya matendo hai kinadharia na kufanya mazoezi ya elimu waliyojifunza darasani.
Mwaka 2015, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi nchini Tanzania iliboresha Mtalaa wa Elimu ya Awali. Hali hii ilitokana na sababu za kudhibiti ubora wa elimu nchini ili kuendana na mabadiliko ya sasa duniani yakiwamo ya sayansi na teknolojia pia kupanua wigo wa elimu. Baada ya kuboresha mtalaa, Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 pamoja na matokeo mbalimbali ya tafiti na mapendekezo kutoka kwa wadau wa elimu, katika Mtalaa wa Elimu ya Awali ikasisitizwa kwamba elimu bora ya awali ni muhimu kwa maisha ya mtoto. Mtoto akijenga msingi imara wa kujifunza katika Elimu ya Awali atakuwa tayari kuanza darasa la 1 na kuendelea vizuri katika ngazi zingine za elimu.

Kwa mujibu wa Sera ya Elimu, lugha rasmi ya kufundishia Elimu ya Awali itakuwa Kiswahili. Lugha ya Kiingereza itafundishwa katika shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia. Vitendo vya Kiswahili vitafundishwa ili kumjengea mtoto uwezo wa kutumia lugha ya Kiswahili. Malengo ya mafunzo ya Elimu ya Awali ni:

i. Kukuza maendeleo ya jumla ya mtoto kiakili, kimwili, kijamii na kihisia;
ii. Kubaini mtoto mwenye mahitaji maalumu na kutoa afua stahiki;
iii. Kumjenga mtoto kimaadili;
iv. Kukuza uwezo wa mtoto wa kuthamini, kudumisha, kujivunia utaifa wake na utamaduni wa jamii yake;
v. Kukuza stadi za awali za ujifunzaji wa mtoto na tabia ya kupenda kujifunza;
vi. Kujenga uwezo wa mtoto kujitambua, kujiamini, kujithamini na kuthamini wengine;
vii. Kukuza urazini wa mtoto katika kutunza mazingira na rasilimali zilizopo;
viii. Kukuza stadi za ubunifu na kufikiri kimantiki; na
ix. Kumuandaa mtoto kujiunga na Elimu ya Msingi (TET, 2017).

Maelezo ya wataalamu tangulizi (Vygotsky, 1980; Levinowitz, 1998; Thornbury, 2002; Suyanto, 2007) yanaonesha kuwa utoto ni wakati muhimu wenye kuzingatia maendeleo ya mtoto. Ni wakati wa kujenga ubongo na mahusiano kuliko miaka yake ijayo. Kwa kadiri nyimbo zinavyotumiwa na namna mitalaa inavyoboreshwa ili kukidhi mahitaji ya watoto katika kufundisha na kujifunza lugha katika elimu ya awali ndivyo watoto wanavyopata fursa ya kuibua ubunifu katika utumizi wa msamiati.

Hivyo basi, utotoni ni kipindi ambacho utembeaji, uzungumzaji, kujithamini, maono na kaida na misingi ya jamii hujengwa. Ni kipindi cha mabadiliko na maendeleo ya mtoto yanayojengwa na matumizi ya muziki unaodhihirika kupitia nyimbo kwa watoto na imethibitishwa kitafiti kama kipindi cha *'muziki wa watoto'* (Gordon katika Levinowitz, 1998). Pia, ni wakati ambao watoto wanauelewa ulimwengu kupitia nyimbo, michezo na lugha (Levinowitz, 1998).

Nadharia ya Vygotsky ya Ujenzi wa Jamii inasisitiza kuwa maarifa ni tofauti na ujifunzaji. Wakati maarifa ni mchakato wa uwili kati ya mtu na mtu katika mazingira akichangamana na wengine (Churcher, Downs na Tewksbury, 2014), kujifunza hutokea kwa mtu mwenyewe katika mifumo ya ndani ya akili kupitia ushirikiano wake na wengine. Kwa hiyo, ujifunzaji huanza katika kiwango cha mtu ambacho ni matokeo ya ujenzi wa maarifa kupitia shirika, na maarifa ni tendo la uwili unaoundwa katika mazingira.

Vygotsky (1980) anaamini kwamba mtalaa bora hauna budi kuhusisha maisha halisi ya uzoefu wa mwanafunzi na kile anachofundishwa. Anaona kuwa lugha na nyimbo vinakua kulingana na mwingiliano wa kijamii, kwa lengo la kuwasiliana. Aliendelea kubainisha kuwa lugha na nyimbo vinaweza kuwa zana bora za wanadamu katika kuwasiliana na ulimwengu wa nje. Kwa mujibu wa Vygotsky, lugha na nyimbo ni mambo yanayoingiliana yenye majukumu kadhaa muhimu katika ukuzaji wa mtalaa kama ifuatavyo:

i. Ni njia kuu ambazo watu wazima huwasilisha maarifa kwa watoto;
ii. Lugha na nyimbo ni vyombo vyenye nguvu inayokubalika akilini;
iii. Lugha na nyimbo ni mambo yanayojengwa na jamii;
iv. Lugha ndio ufunguo wa kuelewa mawazo ya mtu na namna anavyounda maana kupitia namna mbalimbali zikiwamo nyimbo;
v. Lugha na nyimbo ni matendo halisi ya jamii katika kujieleza na kuunda maana, na
vi. Lugha na nyimbo hubadilika kadiri jamii inavyobadilika.

Nadharia ya ujenzi wa jamii huhusishwa na ufundishaji na ujifunzaji wa lugha na nyimbo kwa sababu vitu hivyo viwili hutokana na michakato inayoruhusu kujenga maana kwa namna ya ufundishaji ambao ni changamfu tofauti na ufundishaji ambao ni tulivu. Mwalimu huchukua nafasi ya mwezeshaji kuliko mjuaji wa mambo na hutoa msaada kwa anayejifunza ili aweze kufanya kitu, kumwezesha atende mwenyewe kulingana na maelekezo, akimpa maarifa na kumfanya ajue na kuelewa (Phillips, 2000).

Pamoja na mjadala huo hapo juu, Vygotsky anapendekeza kuwa matokeo ya kujifunza kwa binadamu hutokana na ushirikiano wenye nguvu kati ya mtu binafsi, watu na jamii. Kupitia ushirikiano huo, watoto huweza kujifunza hatua kwa hatua kwa ufanisi na kuendelea kutoka kwa wazazi nyumbani, jamii waliyomo na walimu

shuleni. Kujifunza kunaweza kutofautiana kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kwamba wazo la Vygotsky linasisitiza kuwa lugha na nyimbo ni mazao mwingiliano ya mtu, watu na jamii katika maisha ya uzoefu wao wanaoupata katika mazingira ya utamaduni husika (King'ei, 2010). Hivyo basi, nyimbo za Kiswahili zina nafasi kubwa ya kufundisha msamiati wa lugha katika mtalaa na kufanya ukue na kuenea kama mitalaa itaboreshwa.

## 4.0 Methodolojia ya Utafiti

Kothari (2004) anaeleza kuwa data za kiutafiti hukusanywa na kuhifadhiwa kwa namna mbalimbali. Data za makala haya zilipatikana maktabani na uwandani. Data za maktabani zilipatikana kupitia maandiko na ripoti mbalimbali. Nyaraka hizi zilisomwa kutoka katika Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dodoma, kwenye tovuti na mitandao ya intaneti. Taarifa hizo zilisaidia kufanya nukuu na kuandika marejeleo. Data za uwandani zilipatikana kupitia njia ya ushuhudiaji na usaili.

Ushuhudiaji ulisaidia kupata data za msingi katika mazingira halisi na kukusanya nyimbo nne zilizosaidia kufanya uchambuzi wa aina za msamiati uliofundishwa kwa kutumia michezo ya matendo ya nyimbo mbalimbali walizozifahamu kwa sababu hapakuwa na kitabu maalumu cha nyimbo za watoto. Mwandishi wa makala haya pia ametumia uzoefu wake kama mhadhiri anayefundisha Programu ya Elimu ya Awali katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Mbinu ya usaili ilihusisha walimu wanne na watoto kumi na sita wenye weledi wa nyimbo za Kiswahili ili kubainisha msamiati katika nyimbo hizo. Maswali yalitayarishwa kabla ya mahojiano na maswali mengine yaliibuka papo kwa papo kutegemea na mwelekeo wa mtoataarifa.

Upitiaji wa nyaraka mbalimbali umesaidia kuonesha ushahidi wa matumizi ya nyimbo katika ufundishaji wa msamiati kama sehemu ya matokeo ya utafiti huu. Usampulishaji lengwa wa watoataarifa ulitumika kuwachagua watoataarifa walimu wanne ambapo ilikusudiwa kuona umahiri na kupata weledi wao katika ufundishaji wa madarasa ya elimu ya awali. Pia, watoto kumi na sita walipatikana kwa njia ya usampulishaji lengwa kwa lengo la kupata maudhui ya nyimbo zao zilizoimbwa. Data zilizozaa makala haya zilikusanywa kutoka katika mkoa wa Dodoma (darasa moja) na Geita (darasa moja) ambapo maeneo haya yalichaguliwa kinasibu kama viwakilishi vilivyosawiri namna nyimbo zinavyotumika kufundishia na kujifunzia katika elimu ya awali.

## 5.0 Nadharia Iliyotumika katika Makala

Kuna nadharia kadhaa za lugha ambazo ni pamoja na Umwenendo, Utabia na Uhulka. Utafiti uliozaa makala haya uliongozwa na Nadharia ya Ujenzi wa Jamii iliyoasisiwa na Vygotsky (1980). Mwanazuoni huyu anaamini kuwa maarifa hujengwa kwa mazungumzo na ushirikiano na wengine. Anaendelea kusema kuwa maarifa hupatikana kwa uwili tendaji katika mazingira ya jamii kupitia mchakato wa

uchangamano unaotumia lugha kama chombo kinachojenga maana. Matumizi ya lugha ndicho kiini cha mawasiliano katika kujifunza.

Nadharia ya Ujenzi wa Jamii huona kuwa maarifa si kitu dhahania bali ni matokeo ya utendaji halisi unaoweka mwegamo wa utendaji kwa mwanafunzi kama kitivo cha maarifa. Naye Jin (2011) anaonesha kuwa kutumia Nadharia ya Ujenzi wa Jamii kulileta mafanikio makubwa katika kujifunza lugha ya pili huko China. Mtaalamu huyu alitoa mbinu tano zenye manufaa katika kutumia nadharia hii kama ifuatavyo:

i. *Huamsha hali ya wanafunzi wenye msongo wanaotamani kujifunza lugha.* Kuipokea lugha ni kitu fanisi pale unapofikia mahali ambapo wanafunzi huonesha mambo yanayowapendeza, yanayowapa motisha na kuvumilia tabia zao katika mazingira ya maisha yao. Katika haya wanafunzi wahamasishwe kujifunza lugha, kuvumbua maneno na kushirikishwa katika mijadala na kushiriki utendaji.

ii. *Mwalimu kuongoza mwegamo wa mwanafunzi darasani.* Mwalimu awe mwezeshaji wa tendo la kujifunza lugha kwa kuwaongoza waweze kuona hali ya ulimwengu halisi (Brown, 1994). Watoto wapewe muda wa kuongea zaidi darasani na wasifanywe kuwa hadhira tu.

iii. Kukusanya msamiati wa wanafunzi ili kuwasaidia kuzungumza. Mara nyingi wanafunzi huacha kuzungumza au kuwasiliana kama hawayafahamu maneno lakini yakitumika maneno wanayoyafahamu huongea vizuri zaidi na kujifunza.

*iv.* *Kutumia muda wote wa darasa na kuwafanya wajifunze lugha nje ya darasa.* Wanafunzi wakipewa mazingira bora ya kujifunza lugha ndani na nje ya darasa, hupata muda mzuri zaidi na kuoanisha lugha na mazingira halisi.

*v.* *Kuamsha uelewa wa wanafunzi na utamaduni wa jamii husika*. Kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya lugha na utamaduni na kwamba lugha ni kipengele kimojawapo muhimu cha kuelezea utamaduni. Mwalimu wa lugha anatakiwa atambulishe mila na desturi za jamii mahususi katika kuyatumia maneno ya lugha. Mtu anapojua usuli wa utamaduni wa jamii humwezesha pia kuijia lugha na kuitumia kwa ufanisi na kuielewa.

Mbinu zilizobainishwa zinatuelekeza kuamini kuwa matumizi ya lugha na nyimbo za Kiswahili ambacho ni lugha ya pili kwa walio wengi yanaweza kuwa na matokeo makubwa na kusababisha watoto wakimya kuzungumza na kutumia msamiati mpya. Walimu wakitumia mbinu hizo watatoa fursa kwa watoto kushiriki kutafuta maana ya maneno mapya kwa kuyaeleza wenyewe. Katika kutumia stadi za lugha, mawasiliano hutoka pande zote, yaani kutoka kwa mwalimu na watoto (Mtana, 2003; Oseno, 2010). Mbinu hii humwezesha mwalimu na watoto kuwasiliana kwa urahisi katika tendo la ufundishaji na humrahisishia mwalimu hufanya kazi ya kuongoza majadiliano huku watoto wakiwa ndio wazungumzaji wakuu.

## 6.0 Matokeo na Mjadala

Matokeo ya utafiti uliozaa makala haya yanaonesha kuwa tumezungukwa na nyimbo zenye maudhui tofautitofauti zinazotumika katika kazi za maisha yetu. Katika makala haya tunayajadili matokeo husika kwa minajili ya kujibu maswali/malengo tuliyoainisha kwenye utangulizi. Tumeanza kwa kuainisha aina za nyimbo zinazotoa motisha za kujifunza lugha.

### 6.1 Aina za Nyimbo

Makala haya yamezigawa nyimbo katika makundi makubwa mawili (nyimbo za burudani na nyimbo za kufundishia) ambazo zinatokana na namna nyimbo zinavyotumiwa na kuzingatia ujumbe ulioshuhudiwa katika mazingira ya kufundishia.

**a. Nyimbo za Burudani**

Hii ni aina ya nyimbo pendwa ambazo huimbwa bila maelekezo. Ni nyimbo ambazo watoto huziimba kwa vile huwafurahisha, huzifahamu, huimbika kwa urahisi na huzitumia wanapokuwa nje ya darasa katika matendo yao ya hiari.

**b. Nyimbo za Kufundishia Somo**

Hizi ni nyimbo zinazolenga kufundishia mada mahususi katika somo. Utapofundisha msamiati, nyimbo katika kundi hili hulenga kufundisha matamshi (irabu, konsonanti na silabi), neno (kimuundo) na maneno (sentensi) kama sehemu ya tungo zilivyobainishwa katika mtalaa. Kundi hili la nyimbo huandaliwa na mwalimu kwa ajili ya watoto ili nyimbo hizo zimsaidie katika michakato ya hatua za ufundishaji wake.

Kwa mfano, uchaguzi au utengenezaji ulishuhudiwa kwa kuzingatia vigezo kadhaa katika ufundishaji na ujifunzaji. Baadhi ya vigezo hivyo msamiati unapofundishwa ni kama ifuatanyo:

i. Nyimbo zilitumia neno au maneno yenye maudhui mahususi ya somo;
ii. Nyimbo ziliabiri muundo wa lugha;
iii. Nyimbo zilikuwa na maneno katika muktadha mahususi;
iv. Nyimbo zilielekeza utendaji ulioibua hisia za mwili;
v. Nyimbo zilikuwa mashuhuri ama zilizoelekezwa kwenye mtalaa, na
vi. Nyimbo ziliimbwa kwa furaha na toni amilifu.

Utafiti wa Alemi and Tayebi (2011) wakinukuliwa katika Chulawan na wenzake (2012) ulidhihirisha kwamba kutokuwa na msamiati wa kutosha ni changamoto katika maendeleo ya lugha kwa sababu msamiati ndio kipengele cha msingi katika ujifunzaji wa lugha na humjengea mwanafunzi utendaji wa stadi zingine. Hivyo, ili mtoto aweze kujifunza lugha vizuri anahitaji kuufahamu msamiati unaotumika

katika maisha yake ya kila siku. Njia mojawapo rahisi inayowapendeza katika kujifunza msamiati wa lugha ni matumizi ya nyimbo.

Shule nyingi za elimu ya awali zimeonekana kutumia nyimbo kuelekeza tabia, kufundisha msamiati mpya kwa haraka hasa pale zinapotumika nyimbo pendwa na mashuhuri zinazofahamika kwa muda mrefu (Salcedo, 2010). Yule (1985) anabainisha kuwa mtoto anahitaji maingiliano na watumiaji wa lugha ili ajijenge kwenye lugha husika. Ili mtoto aweze kuitumia lugha na kuimba nyimbo, hana budi aisikie lugha ikizungumzwa na kuzisikia nyimbo zikiimbwa vilivyo. Hivyo basi, ili nyimbo ziweze kuwa na ufanisi ni vema zikawa ni zile zinazoingizwa kwenye matumizi halisi. Kadiri mtoto anavyosikia lugha ikizungumzwa na nyimbo zinavyoimbwa na kuvitumia katika mawasiliano, ndivyo anavyojifunza.

### 6.2 Motisha katika Nyimbo za Kiswahili

Mapitio ya tafiti za wataalamu yanaonesha kuwa motisha ni kitu muhimu kinachoendelea kujadiliwa kwa miaka mingi katika kufundisha na kujifunza lugha. Watafiti na walimu wanaamini kuwa motisha ni muhimu katika upokezi wa lugha kwa sababu wanafunzi wenye motisha ni wale wenye ushiriki changamfu darasani, wanaoeleza matamanio yao kwenye mada za somo na kujifunza kwa jitihada amilifu. Motisha ni kipengele muhimu katika ujifunzaji wenye ufanisi.

Martin (2013) anafafanua kuwa motisha ni hali ya uamshaji wa akili na hisia za mtu anapoongozwa kwenye urazini wa matendo, ambao huamsha fikra au nguvu ya utendaji ili kufikia malengo ya awali. Ikiwa tutayafanya madarasa kuwa sehemu ya furaha kwa mazingira bora ya kujifunzia watoto bila kuwaogopesha, tutawaamshia motisha chanya katika tendo la kujifunza (Nambiar, S, 1985).

Katika hili, nyimbo zinaonekana kufanya vizuri zaidi kwa sababu zina utendaji wenye ujumbe unaoakisi maisha halisia. Nyimbo zina kaida ya kuvutia na kumakinisha wanafunzi ambapo namna zingine za ala elekezi hupungua. Kwa mujibu wa Nambiar, S (1985), mtu ambaye ni kiziwi kabisa kwa wakati fulani anaweza kujifikiria kuwa mwimbaji bora ambapo mtu asiyejua maneno ya wimbo anaweza kukubali namna ya uimbaji wake. Nyimbo zina fursa kubwa ya kurithisha watoto toka kizazi kimoja hadi kingine katika eneo fulani mahalia.

Hata hivyo, kuna wakati ambapo wanafunzi huonekana kuimba nyimbo za kigeni hata kama hawafahamu maneno yake. Hali hii huwapa fursa ya kuwa huru na kuwafanya kujifunza bila shinikizo lolote. Namna hii huzifanya nyimbo kuleta muwala katika tendo la kujifunza na kuboresha mahudhurio darasani hasa pale watoto wanapojifunza wakiwa huria; kwa uhuru na furaha darasani zaidi ya pale wanapojifunza lugha kwa mazingira dhibiti ya kinidhamu.

Huyen na Nga (2003) wanasema kuwa nyimbo huondoa kaida na kwamba ufundishaji wa nyimbo za Kiswahili utaondoa mazingira hatarishi darasani ambapo stadi za lugha zitajengwa kuboresha mahusiano. Nyimbo huwa na mawazo mazito na hutumiwa kuonesha uhusiano wa jamii, migogoro, kukejeli, kuliwaza, kubembeleza, kutumbuiza, kuongoa na kuburudisha (Wamitila, 2003).

Naye Beck (2015) anasisitiza kuwa kutumia nyimbo za watoto ni njia yenye ufanisi kwa watoto wakati wa ufundishaji wa stadi za lugha ili waweze kufurahia na kuitumia lugha. Jambo lingine alilosisitiza katika kazi yake ni mwalimu kufanya mawasiliano kupitia stadi za lugha kuwa jambo la kawaida darasani; hivyo, anatakiwa atoe fursa ya kuwasiliana kwa kuanzisha mada ambayo inahimiza stadi hizo, kuuliza maswali na kubadilishana michango ya mawazo miongoni mwa watoto.

Uimbaji wa nyimbo hujenga roho ya ushirikiano katika kuunda kikundi au vikundi darasa. Hali hii huwasaidia watoto katika utendaji wa stadi za lugha kwa sababu watoto huweza kuimba nyimbo hadi nje ya darasa na kuziimba kwa urafiki katika makundi rika ya wapendwa wao hadi kuzitumia katika mazingira ya nyumbani. Kwa namna nyingine, nyimbo hukazia maarifa ya watoto katika kujifunza lugha. Kwa ufupi, matumizi ya nyimbo huambatisha lugha yenye matamanio au ujumi kubalifu kama tambo muhimu linaloleta mabadiliko yenye motisha katika tendo la kujifunza darasani.

Katika muktadha wa kielimu, wanataaluma hawana budi kuzingatia uhusiano uliopo kati ya muziki, motisha, lugha na ujifunzaji. Makala haya yanajaribu kutoa ushahidi kuwa muziki huwamotisha watoto katika kuwajengea imani ili waweze kujithamini wenyewe, kufanya majaribio magumu wakati wa kujifunza na kujiamini. Hivyo, ni wazi kwamba mtoto kuwa mahiri katika eneo fulani na kujisikia vizuri katika mafanikio ya utendaji wake kwa msaada wa mwingine humsaidia mtoto kurekebisha upungufu wake.

Hata hivyo, kama mtoto fulani atafanya vizuri katika uimbaji, utendaji huo utakuwa wenye nguvu ambukizi kwa wengine na watakaoonekana kutokufanya vizuri katika matumizi ya lugha. Makala haya yanaongeza shuhuda kuwa muziki hutoa msaada kwa wanafunzi wenye udhaifu katika ufaulu kitaaluma na kuwaletea bidii ya ufaulu. Ufahamu binafsi chanya wa muziki kupitia uimbaji huleta ufahamu chanya katika uelewa wa masomo mengine.

Hivyo basi, muziki ni ala ya motisha wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Muziki unaweza kutumika katika ufanikishaji wa malengo yasiyo ya kimuziki. Muziki sanjari na taaluma zingine za kisanaa zisizotumia lugha kama vile uchoraji na uchongaji, hutufikisha karibu na jamii, hutujenga kisaikolojia, hututambilisha kijamii na kukidhi matarajio yetu (Choate, 1968).

Makala haya yanahusisha uimbaji wa nyimbo za watoto katika elimu ya awali, na ujenzi wa dhana za uimbaji unaotokana na uzoefu. Hylton (1981) katika utafiti wake kuhusu uimbaji wa nyimbo na uelewa binafsi alionesha kuwa wanafunzi walifanya tathmini ya uzoefu wao na kusema yafuatayo: i). muziki huwafanya kuwa na uelewa binafsi, ii). muziki huwafanya kujihisi kuwa huru, na iii). muziki huwasaidia kuwa na hali njema ya amani. Aidha, wanafunzi walionesha kuwa na mchangamano muwala katika kiwango cha kijamii, kitu ambacho kiliwajengea uelewa wa jamii yao binafsi.

Makala haya yanazidi kubainisha kuwa muziki na uimbaji ni kiungo na ala muhimu katika tendo la kufundisha na kujifunza lugha ya kwanza au ya pili kwa namna ambayo haitakiwi kudharau10 liwa kama kilivyo Kiswahili nchini Tanzania kuwa lugha ya pili ya wanafunzi walio wengi katika elimu awali. Hylton (1981) alionesha kuwa matumizi ya muziki katika kujifunza lugha ya Kiingereza kama lugha ya pili yaliwamotisha wanafunzi, kufurahia somo kwa uhuru, kutowaingiza katika ushindani kitaaluma na kuwafanya wagundue miundo ya lugha na msamiati mpya katika mawasiliano ya muktadha tofauti.

Qorro (2003) anaelekeza kuwa lugha ya kwanza au lugha inayofahamika vizuri ni chombo cha kumwezesha mwanafunzi kung'amua na kueleza mtazamo na hisia zake za ndani kwa kila kinachomfikia au kinachotolewa kwake. Uwezo huo wa kung'amua na kueleza hisia za ndani kuhusu maarifa anayoyapata, ndiyo msingi wa ubunifu na ugunduzi. Kwa upande wa Tanzania, lugha ya Kiswahili ni ya kwanza kwa baadhi ya watoto na ni ya pili kwa baadhi ya watoto wa elimu ya awali.

Nchini Tanzania, lugha inayotumika kufundishia elimu ya awali ni Kiswahili. Hii ni lugha ambayo inaeleweka wanafunzi wengi ingawa kuna baadhi ya watoto ambao huanza kuitumia lugha hii shuleni ambapo nyumbani hutumia lugha za kijamii. Hali hiyo ya umilisi hafifu wa lugha ya Kiswahili kwa baadhi ya wanafunzi ambao hawana umilisi wa kutosha wa Kiswahili husababisha walimu kukosa uwezo unaostahili wa kufundisha mada kadhaa za elimu ya awali. Kwa hiyo, watoto hulazimika kukariri kwa ajili ya utendaji wao darasani bila kuelewa vema. Hali hii inadai kuwapo na mbinu amilifu ambatizi za ufundishaji kama inavyojadiliwa katika mjadala wa makala haya kuhusu nafasi ya nyimbo na ufahamu wa watoto katika jamii yao ili waweze kujenga maarifa katika kiwango cha elimu ya awali nchini.

Wakifafanua kuhusu nafasi ya Kiswahili, Msanjila na wenzake (2009) wanadai kwamba Kiswahili ni lugha ya taifa na ni lugha rasmi ya shughuli za serikali nchini Tanzania. Lugha hii inatumika pia Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Kenya na Uganda. Aidha, Kiswahili ni lugha ya taifa nchini Kenya. Hata hivyo, Kiswahili kinakubalika na kupendwa kote ulimwenguni kwa namna ambayo baadhi ya vyombo vya habari vya kimataifa hutumia lugha hii kutolea matangazo

kama ilivyo katika vyombo vya habari vya BBC, Sauti ya Amerika na Idhaa ya Kiswahili ya Ujerumani.

### 6.3 Aina za Msamiati na Nyimbo katika Elimu ya Awali

Udurusu wa nyaraka, usaili na ushuhudiaji unaonesha kuwa muziki huhusisha kweli za jamii, matumizi ya lugha yasiyo rasmi ambayo husikika katika uhalisia wake na kuitambulisha jamii. Nyimbo hutoa tunu za thamani ambazo humwendeleza mwanafunzi katika stadi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika (Alemi na Tayebi, 2011; Shrouf, 2014). Kwa mujibu wa Montgomery (2007), kuna aina nne za msamiati. Kuna msamiati wa kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Kila aina ya msamiati imebainishwa katika vipengele vidogovidogo vifuatavyo:

#### a. Msamiati wa Kusikiliza

Haya ni maneno tunayoyasikia na kuyafahamu. Watoto huyasikia na baadaye huweza kujifunza taratibu maneno mapya (Montgomery, 2007). Unapocheza melodia za muziki na nyimbo, watoto wa elimu ya awali huzisikiliza wakati wakifanya kazi kwa namna ambayo huwajengea hali ya kuwa huru na kuchochea ubongo. Hali hii huwatukuza kiakili, kimwili na kuwapa mapigo ya hisia yanayojenga umakini wa kina na kujenga maudhui ya kazi zao vizuri (UNICEF, 2001).

Katika stadi hii, mwalimu wa shule ya awali anatakiwa awaelekeze watoto namna mbalimbali za kutamka irabu, konsonanti au silabi na namna watakavyozibainisha kwenye maneno ya wimbo. Wimbo lazima uwe na maneno watakayoyafanyia kazi. Ni muhimu watoto wabainishe silabi wanazozifahamu au zilizokusudiwa kufundishwa katika wimbo. Kwa vile muziki na lugha hutokana na milio na mapigo yenye mkazo katika maneno, hali hii hukuza stadi ya kusiliza maneno kupitia wimbo bila kusoma.

**Mfano wa wimbo:** “Bainisha Sauti”
Zana: Kanda iliyorekodiwa
*Kokorikooo koo*
*Hii ni sauti ya nini?.......... kuku*
*Meee, meee*
*Hii ni sauti ya nini?........ mbuzi*
*Nyaaau, nyaaau*
*Hii ni sauti ya nini?........ paka*
*Moooo, mooo*
*Hii ni sauti ya nini?....... ng’ombe*
**Chanzo:** Data za Uwandani (2021)

Hatua za kufuata:

i. Mwalimu aongoze watoto katika mkao utakaoruhusu mwitikiaji kujibu;

ii. Mwalimu atambulishe wimbo kwa watoto namna unavyoimbwa na kujibiwa;
iii. Makundi yapangwe kwa namna ya uimbaji wenye ushindani wa kutoa milio
mbalimbali ili wengine watoe jibu la kitu toka katika mlio waliousikia, na
iv. Mwalimu aongoze watoto kuimba nyimbo zingine ambazo mwimbaji ataimba ili wamsilikize na kubainisha msamiati kwa kadiri watakavyoelekezwa (Thornbury, 2002; Montgomery, 2007; Alemi na Tayebi, 2011).

**b. Msamiati wa Kuzungumza**

Watu wana ukomo katika katika idadi ya maneno wanayoyazungumza. Watu wazima huongea maneno kati ya 5,000 na 10,000 katika mazungumzo yao Montgomery (2007). Stadi hii ni muhimu katika kuwafundisha watoto kwa sababu baadhi yao hawawezi kuongea mbele ya wenzao wanapokuwa wanajifunza.

Changamoto ya watoto kutozungumza mbele ya wengine inaweza kuondolewa kupitia matumizi ya nyimbo. Mwalimu anapoandaa wimbo, watoto huuimba katika kikundi na hali hii huwafanya kuzungumza baadhi ya msamiati uliokusudiwa kufundishwa.

**Mfano wa wimbo:** "Najieleza Mama"
Zana: Kanda ya sauti ya wimbo
*Jieleze jieleze jieleze jieleze jieleze jieleze, najieleza Mama. Mimi hapa ni Wambura, Baba yangu ni Samweli, Mama yangu ni Magori Nimejieleza mama.*
**Chanzo:** Data za Uwandani (2021)

Hatua za kufuata katika kufundisha nomino '*baba* na *mama'*

i. Mwalimu apange watoto katika mduara;
ii. Mtoto mmoja ataenda katikati ili ajitambulishe jina lake akionekana kama baba au mama kwa kutumia wimbo wa "Najieleza mama";
iii. Mtoto baba au mama ataingia ndani ya mduara na kujitambulisha kwa jina lake kwa kutumia wimbo tajwa mpaka atakapoona inafaa kulingana na idadi ya watoto, na
iv. Watoto wanaweza kujieleza kwa kutaja majina ya wazazi, majina yao na majina ya ndugu wengine (Mtana, 2003; Montgomery, 2007; Oseno, 2010).

**c. Msamiati wa Kusoma**

Haya ni maneno tunayoyafahamu tunaposoma habari. Kama watoto si wasomaji, hawawezi kufanikiwa kuimudu stadi hii ya kusoma msamiati. Katika stadi hii ya msamiati wa kusoma watoto wanatakiwa kusikiliza muziki kama hatua muhimu ya

maandalizi. Baada ya hapo mwalimu ainue maneno ya wimbo waliousikia katika karatasi kubwa, ubao au kitu chochote kinachowawezesha watoto kusoma.

Iwapo mwalimu anafundisha aina za maneno, atayabainisha kwa kutumia rangi ili ayatofautishe kisha watoto waweze kuyasoma. Baada ya wimbo kuwa umerudiwa na namna mwalimu atakavyoona umefahamika, watoto wanaweza kupewa zoezi la kusoma maneno ya wimbo wenye nafasi iliyoachwa wazi yenye rangi ili wataje aina ya nomino iliyoachwa. Mazoezi ya namna hii yanakuza stadi ya usomaji msamiati kupitia nyimbo. Aidha, mwalimu anaweza kuwaelekeza watoto namna ya usomaji wa maneno kwa kutumia irabu.

**Mfano wa wimbo:** "Hii ndiyo a"
Zana: Picha zenye maneno na herufi za irabu
*Hii ndiyo a, a, a, a ina mkia mfupi a a a*
*ii ndiyo e, e, e, e ipo kama kata e e e*
*Hii ndiyo i, i, i, i ina kofia kichwani i i i*
*Hii ndiyo o, o, o, o ipo kama chungwa o o o*
*Hii ndiyo u, u, u, u, ipo kama kikombe u u u*
**Chanzo:** Data za Uwandani (2021)

Hatua za kufuata wakati wa kutumia stadi ya kusoma:

i. Mwalimu aongoze watoto waimbe wimbo wa 'Hii ndiyo A' unaotaja irabu akisoma na kuhusisha neno, kitu halisi au picha husika toka kifungu cha habari ya wimbo alichopewa;
ii. Watoto wasome maneno ya wimbo katika kadi wakihusisha na irabu zilizosomwa;
iii. Watoto wasome maneno kisha wabainishe irabu, na
iv. Mwalimu awape watoto kadi za maneno yenye picha za vitu vinavyoanza na irabu fulani, kisha waoanishe picha za vitu na kadi za irabu kwa kutamka silabi (Montgomery, 2007; Schmitt, 2010; Shrouf, 2014).

### d. Msamiati wa Kuandika

Msamiati wa kuandika ni maneno tunayoandika wakati wa kujieleza wenyewe. Maneno tunayoandika mara nyingi ni yale yanayotokana na matamshi yetu (Montgomery, 2007). Katika stadi hii, mwalimu anatakiwa acheze wimbo kwa wanafunzi wake. Baada ya hapo, anaweza kuwapa makala ya wimbo ikiwa na nafasi zilizoachwa wazi yenye maneno yanayokosekana.

Mwalimu acheze wimbo mara kadhaa kwa namna atakavyoona inaeleweka. Baadaye, watoto watapewa karatasi ya maneno ya wimbo yaliyoachwa wazi ili wajaze. Pia, wanaweza kuwekewa wimbo wausikilize, baadaye waandike hadithi fupi wakitakiwa watumie wimbo waliousikiliza. Wanaweza kubainisha aina za maneno kama vile nomino, vitenzi na kadhalika kwa namna mwalimu atakavyoona

ni mwafaka. Namna hii huchochea watoto waweze kukuza stadi ya kuandika kwa kutumia nyimbo wanazozifahamu na kuzifurahia.

> **Mfano wa wimbo:** "Tuamkapo Asubuhi"
> **Vifaa:** Kibao chenye maneno ya wimbo
> *Tuamkapo asubuhi tuwasalimu wazazi, shikamoo baba, shikamoo mama, hiyo ndiyo tabia njema. Tuendapo masomoni tuwasalimu walimu, shikamoo mwalimu, shikamoo mwalimu, hiyo ndiyo tabia njema. Tukutanapo katika michezo tuwasalimu wenzetu, hujambo rafiki, sijambo rafiki, hiyo ndio tabia njema.*
> **Chanzo:** Data za Uwandani (2021)

Hatua za kufuata katika kufundisha msamiati katika stadi hii:

i. Watoto waanze kwa kuimba wimbo wa kusalimiana;
ii. Wasomewe maneno ya wimbo mara kadhaa ili wabainishe wazo kuu;
iii. Washirikiane katika vikundi ili waoneshe namna za salamu kwa kutaja majina ya watu mbalimbali yaliyoandikwa, na
iv. Watoto wapewe kazi ya kuandika aina za maneno fulani au habari fupi kuhusu salamu (Murphey, 1992; Thornbury, 2002; Montgomery, 2007; Alemi na Tayebi, 2011).

Kwa ujumla, matumizi ya nyimbo katika kufundishia msamiati wa lugha ni njia fanisi ya kujenga uelewa wa lugha kwa watoto katika elimu ya awali. Maneno wanayoyasikia katika nyimbo, kuyazungumza, kuyaandika na kuyasoma wakizingatia matamshi, mkazo na viimbo huwajengea uwezo mkubwa wa kujifunza katika masomo yote (Murphey, 1992).

### 6.4 Mbinu za Kufundishia Msamiati

Udurusu wa nyaraka umeonesha kuwa kuna mbinu kadhaa za kufundishia msamiati ambazo baadhi yake zinaweza kutumia nyimbo ili kufanikisha ujifunzaji. Mbinu hizo si muhimu kwa mwalimu tu bali pia ni mbinu zinazomwezesha mtoto wa elimu ya awali kujenga uwezo wa kuitumia lugha. Baadhi ya mbinu hizo ni:

#### a. Vielelezo vya Kuona

Katika mbinu hii mwalimu anaweza kutumia karatasi iliyoandikwa maneno ya wimbo au kibao cha mwanafunzi. Mwalimu anatumia maneno ya wimbo katika karatasi au ubao wa mtoto kisha anapigia mstari msamiati anaoutaka. Mojawapo ya kielelezo cha kuona ni kibao. Mwalimu anaweza kukitumia kwa kuandika maneno na maana zake ili kufundishia msamiati.

Stokes (2002) anabainisha kuwa vielelezo vya nyimbo za kuona humsaidia mtoto kujifunza msamiati wakati huohuo akihusisha maneno kupitia picha anazoziona. Picha hizo husaidia kuibua uelewa wake wa awali na kutoa maelezo mazuri juu ya

msamiati anaojifunza kuliko kutegemea somo la maelezo tu. Utamkaji wa msamiati unaweza kuwa mzuri zaidi endapo mtoto atajifunza kwa kuangalia nyimbo za picha kama kielelezo amilifu. Hata hivyo, endapo mwalimu atapata changamoto ya kuzipata nyimbo za picha katika kufundishia msamiati anaweza kuziperuzi katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na intaneti.

**b. Maelezo ya Mdomo**

Katika mbinu hii, mwalimu anachagua msamiati anaotaka kufundisha na kuandaa kulingana na kiwango cha maendeleo ya watoto, lengo lililokusudiwa na kuzingatia muda uliopangwa katika kujifunza. Matumizi ya mbinu hii ni ya haraka na yenye ufanisi kwa mwalimu katika kufundisha msamiati kwa urahisi katika kuelezea msamiati mpya. Japokuwa mbinu hii ni ya haraka, huonekana kutowafurahisha watoto kwa sababu haina viambata vingine vinavyoibua motisha katika tendo la kujifunza.

Mara nyingi, njia ya maelezo hutolewa kwa namna ya mhadhara ambao hujikita katika maelezo tu. Mhadhara katika madarasa ya watoto wa elimu ya awali ambayo yanahitaji utendaji zaidi huonekana kutowashirikisha watoto katika tendo la kijifunza na hivyo huwachosha na kuonekana siyo njia shirikishi. Mwalimu anapotumia mbinu hii, anaweza kuihusisha na mbinu zingine ambazo huibua motisha kwa watoto ikiwa ni pamoja na matumizi ya nyimbo.

**c. Kubuni katika Muktadha**

Katika mbinu hii mtoto anajifunza msamiati kutoka kwenye kifungu cha habari. Msamiati unaweza kubainisha maana kwa namna ulivyotumiwa katika maneno ya wimbo kwa kuonesha maana iliyoibuliwa. Njia hii ni nzuri kwani huangalia maana kimatumizi katika utendaji halisi bila kutumia kamusi. Mbinu hii ni fanisi kwa mwanafunzi na mwalimu kwa sababu hujenga tabia ya udadisi na kufikiria jambo la msamiati fulani kwa kina.

Mbinu ya kubuni katika muktadha inaweza kuwa ya msaada kwa mwalimu endapo ataandaa wimbo wenye msamiati wa kutosha wa watoto kujifunza. Mtoto anaposikia wimbo na kisha kupata orodha ya maneno asiyoyajua, humfanya atafute maana ya maneno hayo kwa kuuliza wenzake. Hii humjenga mtoto kijamii na kiakili. Mwalimu anaweza kuwagawa watoto katika makundi madogomadogo ili wajenge fikra tunduizi zenye bunio katika kupata maana ya msamiati waliyopewa.
Matokeo yaliyojadiliwa hapo juu yanatuelekeza kuamini kuwa:

i. Nyimbo zina ushawishi katika ufundishaji wa msamiati ya Kiswahili;
ii. Walimu wanapaswa kuchagua nyimbo za kufundishia kwa umakini mkubwa;
iii. Nyimbo zitakazochaguliwa ziende sambamba na uwezo wa umri na kiwango halisi cha maendeleo ya lugha ya mtoto;
iv. Matumizi ya nyimbo huibua ubunifu katika kutumia msamiati;

v. Kabla ya watoto kusikililiza wimbo, mwalimu hana budi awe ameupitia na kurekebisha makosa ya kisarufi katika maneno yake;
vi. Mwalimu anaweza kutumia wimbo kwa kutoa kazi za nyumbani ili watoto wabainishe msamiati katika nyimbo walizopewa;
vii. Uimbaji ni kitu kinachopendwa na watoto na kinapotumiwa darasani huwachangamsha;
viii. Watoto wanaweza kutumia wimbo zaidi ya mmoja ili wajifunze kwa ufanisi;
ix. Watoto hupendelea kujifunza lugha kwa kutumia vifaa anuwai vinavyovutia;
x. Watoto hupendelea kujifunza msamiati kwa kamusi zinazotoa sauti zenye mahadhi ya muziki au nyimbo;
xi. Uimbaji huwafanya watoto wajifunze kwa uhuru na hivyo mwalimu anaweza kuwaandaa watoto akianza na nyimbo, na
xii. Watoto wanaweza kujifunza msamiati mpya kwa kutumia nyimbo (Suyanto, 2007; Montgomery, 2007; Kao na Oxford, 2014).

Kwa ujumla, mjadala umebainisha kuwa nyimbo ni muhimu katika jamii kwa sababu hutambulisha jamii kwa kusawiri shughuli na maisha ya jamii iliyozibuni. Nyimbo ni njia mojawapo ya kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii. Aidha, nyimbo hutumiwa kufundishia na kujifunzia amali na mambo ambayo jamii inayathamini mtoto ayapate kupitia lugha katika elimu ya awali. Kupitia nyimbo, tamaduni, maadili na elimu huakisiwa na hivyo jamii au taifa linakuwa limetambulishwa.

## 7.0 Hitimisho

Kwa ujumla, nyimbo zimeonesha kujenga tabia zenye mwenendo chanya na motisha kwa watoto katika ufundishaji na ujifunzaji wa msamiati wa lugha ya Kiswahili. Watunga sera, wakuza mitalaa, walimu na wazazi hawana budi kuhakikisha kuwa mtoto kama mtu binafsi katika kundi jamii anahitaji kuandaliwa ili apate maarifa halisi ya jamii, kuzitatua changamoto za mazingira katika jamii au taifa lake na kumkuza kwa ukamilifu wake. Matumizi ya muziki kupitia nyimbo yana ufanisi mkubwa katika kumwandaa mtoto kupata maarifa ya elimu ya awali.

## Marejeleo

Agu, D.C.C. (2006) "The Nigerian Policy on Education: Its impact on music education programme and delivery in Nigeria". *Awka Journal of Research in Music and the Arts (AJRMA)*. Juz. 3: 1-8.

Alemi, M. na Tayebi, A. (2011) "The influence of incidental and intentional vocabulary acquisition and vocabulary strategy use on learning L2 vocabularies". *Journal of Language Teaching and Research*, 2(1).

Arevalo, E.A.R. (2010) "The Use of Songs as a Tool to Work on Listening and Culture in EFL Classes". Inapatikana katika https://www.redalyc.org/pdf/3222/322227521008.pdf. Ilisomwa tarehe 17.12.2015.

Beck, D. (2015) Linkedin Corporation, 12.2.2015.
Blacking, J. (1973) *How Musical is Man?* London: Faber & Faber.
Brown, A.L. (1994) "The Advancement of Learning". *Educational Researcher* Juz. 23: 4-12.
Bruner, J.S. (1966) *Toward a Theory of Instruction*. Cambridge: Mass.: Belknap Press of Harvard University. Inapatikana katika http://datad.aau.org/... /15BIBLIOGRAPHY.PDF. Ilisomwa tarehe 03 Januari 2016.
Choate, R.A. (1968) "Documentary report of the Tanglewood Symposium". Reston, VA .1-4. https://www.bu.edu/tanglewoodtwo/about/documentreport.pdf. Ilisomwa tarehe 05 Februari 2021.
Churcher, K.M.A., Downs, E. na Tewksbury, D. (2014) "Friending" Vygotsky: A Social Constructivist Pedagogy of Knowledge Building through Classroom Social Media Use. *The Journal of Effective Teaching,* 14(1): 33-50. Inapatikana katika http://uncw.edu/cte/et/articles/Vol14_1/Churcher.pdf. Ilisomwa tarehe 12 Januari 2016.
Davanellos, A. (1999) "Songs". *English Teaching Professional,* Juz. 13: 13-15.
Ekpo, I. S. (2008) "Parental Factor in Early Musical Exposure as a Prerequisite for Ideal Musical Development of the Child": Nigeria's Experience. *Awka Journal of Research in Music and the Arts (AJRMA)*. Juz. 5: 26-34.
Esimone, C.C. (2012) *Music in Early Childhood Education: A Study of Selected Preprimary Schools in Anambra State, Nigeria*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nnamdi Azikiwe, Anambra
Huyen, N. na Nga, K. (2003) "The Effectiveness of Learning Vocabulary through Games". *The Asian EFL Journal*. Inapatikana katika ttps:// www.researchgate.net/publication/311689467_Improving_Students'_Vocabulary_Achievement_through_Word_Game. Ilisomwa 12.01.2020
Hylton, J. B. (1981) "Dimensionality in High School Students Participants' Perception of the Meaning of Choral Singing Experience". *Journal of Research in Music Education*, Juz. 29, 287-303.
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2014) *Sera ya Elimu na Mafunzo*. Dar es Salaam: Wizara ya Elimu na Utamaduni.
King'ei, K. (2010*) Misingi ya Isimujami*. Dar es Salaam: TUKI.
Kothari, C. (2003) *Research Methodology – Methods and Techniques* (2nd Ed) London: University of Nevada.
Jin, L. (2011) "Constructivism: Application in oral English Teaching to Non-English Majors". *Global Partners in Education Journal*, Juz. 1(1):13-20. Inapatikana katika www.gpejournal.org/index.php/GPEJ/article/view/. Ilisomwa 02 Januari 2016.
Kao, T.A., na Oxford, R.L. (2014). Learning Language through Music: A Strategy for Building Inspiration and Motivation. *System*, Juz. 43: 114-120.
Kasuwan, M. na Chatuphot, M. (2013) "Effectiveness of English Song Activities on Vocabulary Learning and Speaking Ability and Retention" *Journal of Liberal Arts*. Juz. 5: 2.

Levinowitz, L.M. (1998) The Importance of Music in Early Childhood Education. In the General Music Today. Music Educator's National Conference. Inapatikana katika http://www.musictogether.com/Import. Ilisomwa 26 Aprili 2014.

Martin, C. (2013) "The Effects of Songs in Foreign Language Classroom on Vocabulary Retention and Motivation." Inapatikana katika https://academicae.unavarra.es/xmlui/bitstream/handle/2454/9828/master%201.pdf?sequence=1&isAllowed=y. Ilisomwa 14 Desemba 2015.

Msanjila, P.Y., Massamba, D.P.B. na Kihore, Y.M. (2009) *Isimujamii Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam. TUKI.

Ministry of Education and Culture, (MOEC, 2005) *Education and Training Policy*. MOEC, Dar es Salaam. Inapatikana katika http://www.tzonline.org/pdf/Educationandtrainingpolicy. Ilisomwa tarehe 24.04.2016.

Montgomery, J.K (2007) *The Bridge of Vocabulary*: Evidence Based Activities for Academic Success. USA: NCS Pearson Inc.

Mtana, N. (2003) *Ufundishaji Unaozingatia Ujenzi wa Maana*. Dar es Salaam: Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Mulokozi, M.M. (1996) *Fasihi ya Kiswahili*, Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Murphey, T. (1992) *Music and song*. Oxford: Oxford University Press.

Nambiar, S. (1985). The use of pop songs in language learning. *Guidelines* 7(1):79-87.

Nyerere, J., (1968) *Freedom and Socialism:* A Selection from Writings and Speeches, 1965–1967. Oxford University Press, Dar es Salaam.

Oseno, B. (2014) Teaching Speaking Skills: Challenges of Using Integrated Approach in Secondary Schools. (pdf).

Philips, D.C. (2000) *Constructivism in Education*. Chicago: IL: University of Chicago Press.

Prescott, J.O. (2005) "Music in the Classroom: Instructor's Handy Guide for Bringing Music into your Classroom." iCyte. Inapatikana katika http://www.icyte.com/system/snapshots/fs1/7/1/d/5/71d50975596ee47687f4be608 d50ccfc3. Ilisomwa 01 Aprili 2021.

Qorro M.A.S. (2003) "Unlocking Language Forts. in The Language of Instruction in Post Primary Education in Africa with Special Reference to Tanzania." Katika B. Brock-Utne, Z. Desai and M. Qorro (Wah.) *Language of Instruction in Tanzania and South Africa.* (hakuna mji) E&D Limited.

Salcedo, C. S. (2010) "The Effects of Songs in the Foreign Language Classroom on Text Recall, Delayed Text Recall and Involuntary Mental Rehearsal". *Journal of College Teaching & Learning.* Juz. 6: 19-30.

Schmitt, N. (2010) *Researching Vocabulary*: A Vocabulary Research Manual. Palgrave Press.

Shrouf, F. (2014) *Teaching and Improving Speaking Skill*. Philadephia University. Education, Zanzibar. Educational Publishers, London.

Stokes, S. (2002) “Visual Literacy in Teaching and Learning”: A Literature Perspective. *Electronic Journal for the Integration of Technology in Education*. Juz. 1 (1): 10-19. Inapatikana katika http://ejite.isu.edu/volume1no1/pdfs/stokes.pdf. Ilisomwa 03.02.2018

Suyanto, K.K.E. (2007) *English for Young Learner*. Jakarta: Bumi Aksara.

Tassoni, P. na Hucker. K. (2000) *Planning Play and the Early Years*. Oxford: Heinemann Educational Publishers.

Taasisi ya Elimu Tanzania (2017) *Mwambata wa Kufundishia Elimu ya Awali.* Dar es Salaam.

Thornbury, S. (2002) *How to Teach Vocabulary*. Harlow: Longman.

UNICEF (2001) Early Childhood Development: The Key to a Full and Productive Life. Inapatikana katika http://www.unicef.org/dprk/ecd.pdf. Ilisomwa 18.07. 2020

Vygotsky, L.S. (1980) *Mind in Society: The Development of Higher Psychological Processes*. Harvard University Press.

Wamitila, K.W. (2003) *Kamusi ya Fasihi*: *Istilahi na Nadharia*, Nairobi: Focus Publications Ltd.

Walker, R. (1998) “In Music Education, a Hundred Flowers Blossom and a Hundred Schools of Thought Contend. Is this a Problem?” *International Journal of Music Education* (IJME), Juz. 1: 32-34.

Yule, G. (1997) *The Study of Language*. Cambridge: University Press.